

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA
MKAKATI WA WILAYA WA KUKABILIANA NA MAAFA MBALIMBALI
UTANGULIZI.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi ambayo yamekuwa yakitokea kwa kasi sana. Miongoni mwa Mabadiliko ya Tabia ya Nchi imekuwa ni kuongezeka kwa joto katika maeneo ambayo hali hiyo ilikuwa siyo kawaida, Kupungua na kuongezeka kwa kiwango cha mvua na hata kipindi cha kunyesha mvua hizo, kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai.

Mabadiliko haya ya Tabia ya nchi yamesababishwa na mambo mengi. Miongoni mwa hizo ni shughuli za kibinadamu kama Kilimo, Ufugaji, Ukataji miti hovyoy, shughuli za ujenzi, uchimbaji madini na kukua kwa teknolojia kama ongezeko la mitambo mbalimbali ambayo inasababisha kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa hali ya hewa na maji.

Mabadiliko ya Tabia ya nchi yamesababisha madhara mbalimbali. Madhara hayo ni pamoja na vipindi virefu vya jua vinavyopelekea kuwepo kwa Ukame, kutokea kwa mafuriko, Vifo vya binadamu na wanyama, Kuongezeka kwa joto katika maeneo mbalimbali, upungufu wa chakula na kupelekea njaa, kukauka kwa vyanzo vya maji.

Wilaya ya Kyerwa mwaka 2016/17 ilipata madhara makubwa ya mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kupata kipindi kirefu cha jua ambacho kilipelekea mazao mengi kukauka na kusababisha upungufu wa chakula kwa kaya nyingi. Hii ilipelekea Wilaya kuwa na uhitaji wa msaada kwa upande wa chakula. Zaidi ya 50% ya kaya zote Wilayani Kyerwa ziliathirika na hali hii. Pamoja na Ukame uliojitokeza pia Tetemeko la Ardhi la Septemba 10, 2016 lilisababisha madhara makubwa kwa kuharibu makazi ya watu na majengo ya Taasisi mbalimbali. Ilikuwa ni mara kwanza kwa Wilaya ya Kyerwa kukumbwa na majanga hayo kwa kipindi cha miaka mingi. Hii ilipelekea wananchi kukumbuka kuwa wakati wowote majanga hutokea hivyo kujiandaa kukabiliana nayo.

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa pia imejipanga kuhakikisha inajiandaa vyema kuabiliana na Maafa mbalimbali yanayosababishwa na Mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na majanga ya asili kama tetemeko, Mafuriko na kimbunga. Jedwali hapo chini linaonesha jinsi Wilaya ilivyojiandaa kukabiliana na majanga mbalimbali yanayoweza kujitokeza.

Jedwali: Majanga na namna ya kukabiliiana nayo

JANGA	NAMNA YA KUKABILIANA NALO
<p>1. UKAME/NJAA</p>	<p>1. Halmashauri imetenga fedha kupitia Idara ya Kilimo kwa ajili ya kukabiliiana na janga la njaa kwa namna tofauti. Kwanza imenunua na kusambaza mbegu za viazi kwenye kaya na taasisi kwa ajili ya kukabiliiana na njaa, lakini pia kutoa elimu na kufanya tathmini ya kuhakikisha kila kaya inahifadhi chakula cha kutosha kabla ya kuuza kinachozidi.</p>
	<p>2. Halmashauri imehamasisha kila kaya kutenga walau robo ekari kwa ajili ya kilimo cha mazao ya kinga ya njaa (Mihogo na Viazi) na kuanzisha miradi ya kilimo kwa ajili ya kinga ya njaa</p>
	<p>3. Mkurugenzi Mtendaji ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ya Wilaya ameelekeza viongozi wa ngazi za chini (Kata na vijiji) kukutana na kufanya tathini kwa vipindi vilivyoainishwa katika miongozo.</p>
<p>2. MAGONJWA YA MLIPUKO</p>	<p>1. Halmashauri imeendelea kuelimisha wananchi kukabiliiana na magonjwa ya mlipuko kupitia vituo vya afya na zahanati.</p>
	<p>2. Idara ya mifugo imeweka mikakati ya kutoa elimu ya magonjwa ya mlipuko kwa mifugo na kufanya chanjo kwa ratiba ili kuzuia magonjwa hayo. Mbali na hiyo imekuwa ikiweka vizuizi vya kusafirisha mifugo kunapohisiwa kuna ugonjwa wamlipuko.</p>

	3. Aidha mkakati wa kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo bora unaendelea
	4. Mkurugenzi Mtendaji ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ya Wilaya ameelekeza viongozi wa ngazi husika kukutana na kufanya tathini kwa vipindi vilivyoainishwa katika miongozo
	5. Halmashauri kupitia Vituo vya Afya na Zahanati inaendele kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji endelevu wa dawa na vifaa tiba
3. MAJANGA YA ASILI (TETEMEKO, MAFURIKO, KIMBUNGA N.K)	1. Halmashauri kwa mwaka huu wa fedha haijatenga maeneo kwa ajili ya kuwahamishia wahanga endapo maafa yatatokea lakini hali ikitokea Halmashauri imejipanga kutumia taasisi mbalimbali za serikali vikiwemo vituo vya afya na zahanati kwa ajili ya kukabiliana na Maafa yatakapotokea
	2. Watendaji katika ngazi za Kata na vijiji wameelekezwa kuwasisitiza wananchi waishio maeneo hatarishi kuhamisha makazi yao kabla ya kutokea kwa maafa.
	3. Mkurugenzi Mtendaji ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ya Wilaya ameelekeza viongozi wa ngazi husika kukutana na kufanya tathini kwa vipindi vilivyoainishwa katika miongozo.

Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa pia imejipanga kuhamasisha wadau mbalimbali wa Maendeleo kwa ajili ya kusaidia kuokoa na kurejesha hali mara Maafa yanapojitokeza. Hii itafanyika kwa kupitia mikutano mbalimbali na wadau wa maeneo mbalimbali ndani nan je ya Wilaya.